

MATOKEO YA AWALI YA PATO LA TAIFA KWA ROBO MWAKA, OKTOBA – DESEMBA 2015


Ofisi ya Taifa ya Takwimu ina jukumu la kukusanya, kuchakata na kusambaza takwimu rasmi za kiuchumi na kijamii Nchini. Takwimu hizi ni pamoja na takwimu za Pato la Taifa kwa robo Mwaka na kwa mwaka mzima.

Pato la Taifa kwa robo mwaka ni thamani ya bidhaa na huduma zilizozalishwa nchini katika vipindi vya miezi mitatu mitatu ambavyo ni Januari – Machi, Aprili – Juni, Julai – Septemba na Oktoba - Desemba. Takwimu za Pato la Taifa hujumuisha shughuli zote za kiuchumi.

Katika kipindi cha cha robo ya nne ya mwaka (Oktoba hadi Desemba) 2015, matokeo ya awali ya takwimu za Pato la Taifa kwa robo mwaka kwa bei za miaka inayohusika yameonesha kuwa thamani ya Pato la Taifa ilikuwa Shilingi trilioni 22.9 ikilinganishwa na Shilingi trilioni 19.1 ya kipindi kama hicho mwaka 2014.

Thamani ya Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2007 katika kipindi cha robo mwaka ya nne ilikuwa Shilingi trilioni 10.9 kwa mwaka 2015 ikilinganishwa na Shilingi trilioni 10.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2014, hii inamaanisha kuwa Pato la Taifa liliongezeka kwa kasi ya asilimia 7.1 katika kipindi cha robo ya nne mwaka 2015 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 4.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2014 (Kielelzo Na.1).

Kielelezo Na. 1: Kasi ya Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Robo ya Nne, Oktoba - Desemba, 2006 – 2015



Katika kipindi cha Oktoba – Desemba, 2015 shughuli za kiuchumi ambazo zimekua kwa kasi kubwa zaidi ni pamoja na Habari na Mawasiliano (asilimia 23.0),

Utawala na Ulinzi (asilimia 19.7), Huduma za Fedha na Bima (asilimia 13.6) na Madini na Uchimbaji Mawe (asilimia 10.6).

Aidha, katika kipindi hiki, shughuli za kiuchumi ambazo zimekua kwa kasi ndogo ni pamoja na Umeme (asilimia 0.1), Maji (asilimia 1.4), Malazi na Huduma za vyakula (asilimia 1.7) na Kilimo asilima 2.6.

Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, matokeo ya awali ya takwimu za Pato la Taifa kwa mwaka 2015 kwa bei za miaka inayohusika yameonyesha kuwa thamani ya Pato la Taifa mwaka ilikuwa Shilingi trilioni 94.6 ikilinganishwa na Shilingi trilioni 79.4 mwaka 2014.

Thamani ya Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2007 katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2015 ilikuwa Shilingi trilioni 44.1 kwa mwaka 2015 ikilinganishwa na Shilingi trilioni 41.2 mwaka 2014, sawa na ongezeko la asilimia 7.0 mwaka 2015 ikilinganishwa na ukuaji kama huo wa asilimia 7.0 mwaka 2014.